JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA

Tovuti: www.hlpc.go.tz

# TANGAZO

## MABORESHO YA MFUMO WA HPRS SEHEMU YA "CPD"

Baraza linawatangazia Wataalam wa Maabara kuwa limefanya maboresho ya mfumo wake wa HPRS katika moduli ya "CPD" kama ifuatavyo;

- Mfumo wa HPRS katika moduli ya "CPD" imeunganishwa na mfumo wa E-learning hivyo alama za "CPD" zitakazopatikana baada ya kusoma na kupata cheti katika fumo wa E-learning zitatumwa moja kwa moja kwenye account ya Mtaalam bila kufanya maombi (By Claiming).
- Mafunzo yote ya E-learning hayatahitaji kufanya maombi kabla ya kusoma (apply session), Mtaalam atafungua sehemu ya View (iliyoko mbele ya kipindi husika) na kubonyeza "link" itakayompeleka moja kwa moja kwenye mfumo wa E-learning akasome na alama zitatumwa kwenye akaunti yake.
- Mfumo wa HPRS umewezeshwa Mtaalam kufanya maombi zaidi ya mara moja baada ya maombi ya awali kukataliwa (Re-claim points)
- Mfumo wa HPRS umewezeshwa Mtaalam kuomba zaidi ya mara moja kwenye aina moja ya shughuli ya mafunzo (Activity Category)
- Mfumo wa HPRS umewezeshwa kuondoa vipindi ambavyo muda wake umeisha katika sehemu ya "Session available" hivyo kumpatia wepesi Mtaalam kuona vipindi vya siku husika. Aidha, Mtaalam ni lazima abonyeze neno "apply" kabla ya kipindi kuanza, vinginevyo hatoweza kukiona kipindi hicho baada ya tarehe ya mafunzo kupita.
- Mfumo wa HPRS umewezeshwa kutafuta kipindi (Search) sehemu ya "session available " kwa kuandika jina la kipindi husika
- Mfumo umewekewa sehemu ya Mtaalam kuangalia idadi ya alama za CPD kwa kila mwaka wa fedha wa serikali

Aidha, Baraza linawasisitiza Wataalam kuendelea kukusanya alama za CPD zitakazowawezesha kuhuisha leseni zao kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kadiri ya mwongozo wa Baraza wa Mafunzo endelevu (HLPC CPD guidline; 2022).

Baraza linatarajia kufanya mafunzo ya kimtandao (zoom) kuhusu mabadiliko haya kwa kufuata ratiba iliyoambatanishwa hapa chini.

Nawatakia utekelezaji mwema.

Imetolewa na ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara.
27/11/2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
RECEIVED
27 NOV 2024
P.O.Box 743
DODOMA

Scanned with CamScanner

**RATIBA YA MAFUNZO YA MODULI YA "CPD" KWENYE MFUMO WA HPRS**

| Tarehe | Muda | Kanda |
|---|---|---|
| 29.11.2024 | Saa 2:30 Asubuhi | Kanda ya Magharibi |
| | | Kanda ya Kasikazini |
| 02.12.2024 | Saa 8 mchana | Kanda ya kati |
| | | Kanda ya Ziwa |
| 03.12.2024 | Saa 10 jioni | Kanda ya Nyanda za Juu kusini |
| 05.12.2024 | Saa 9 alhasiri | Kanda ya Mashariki |



Scanned with CamScanner